# UNAMJUA HUYU?

**Tamthiliya**

MWANAWETU MMUNI

**Hakimiliki ©Mwanawetu Mmuni**
Mwanawetu Mmuni
P. O Box 90,
Mtwara – Tanzania
Simu; +255 737966996

Chapa ya kwanza 2020
e-Book
Lulu Selfpublishers

© 2021

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kufasiri, kuchapa, au kutoa kitabu hiki kwa njia yeyote ile bila idhini ya Mwandishi.

**Vitabu vya Mwanawetu Mmuni tangu 2017**

1. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 1
2. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 2
3. Usimwache atoke “Don’t let him go out” 3
4. Hasira ni hasara
5. A life after Beijing
6. Jumanne katika msitu wa maajabu
7. Kilimo chetu: Karibu sherehe za Nanenane ki-taifa Lindi 2017
8. **Unamjua huyu?**
9. Come with me
10. Dharau
11. Imani yangu
12. Ken na Kandi
13. JIFIKIRIE
14. NIFIKIRIE
15. Nadharia ya maisha ya mti na mtu
16. Falsafa Mtandaoni
17. Safari ya Mikumi
18. Mwenge wa Uhuru na Ukombozi wa Fikra
19. Mzigo wa jirani
20. Hadithi za karne ya 21
21. Elimu mtaani
22. Chumbani
23. Umebadilika
24. Kiburi chaponza kichwa

# YALIYOMO

IGIZO .......... **Error! Bookmark not defined.**

YALIYOMO .......... 4

UTANGULIZI .......... 5

Wahusika .......... 6

SURA YA KWANZA .......... 7

Nyumbani .......... 7

SURA YA PILI .......... 12

Gharama ya siri .......... 12

SURA YA TATU .......... 22

Pendo .......... 22

Raha ya kazi .......... 26

SURA YA NNE .......... 32

Utaweza? .......... 32

SURA YA TANO .......... 39

Subra .......... 39

SURA YA SITA .......... 51

Ni huyu? .......... 51

# UTANGULIZI

Tamthilia hii inawahusu wanandoa wawili; Jesca na Kelvin. Wanaishi Mbezi Beach kwenye nyumba yao ya kifahari. Katika miaka kumi ya ndoa yao; wamebahatika kupata mtoto mmoja. Muda mwingi mtoto huyo anakosekana nyumbani na kubakia na wafanyakazi wao wa ndani pekee kwa sababu anasoma Shule ya bweni.

Jesca alitambulisha kazi yake ni Meneja masoko katika kampuni binafsi jijini Dar-es-salaam wakati Kelvin ni Mfanyabiashara wa magari, vipuri vya magari, na vifaa vya umeme kutoka nchi za nje hasa China na Japan. Ingawa walikuwa wanafanyakazi hizo zinazotambulika, lakini kila mmoja alikuwa na kazi nyingine ya siri.

## Wahusika wakuu

1. Jesca
2. Kelvin
3. Kesi
4. Kanu

## Wahusika wengine

5. Nasra
6. Mama Nasra
7. Mlinzi wa familia ya Kelvin
8. Katibu wa Jesca
9. Mlinzi wa hoteli

# SURA YA KWANZA

## Nyumbani

Familia imekumbwa na wingi wa kazi na kila mmoja anapofika nyumbani anakuwa amechoka.

**Usiku, Jesca na Kelvin**

Wanaonekana wapo chumbani wamelala. Muonekano wa chumba ni wa kupendeza kwa kuwa ni kusafi sana na huwepo wa mng'aro wa mapambo ya kuvutia. Anayewaona anaweza kuhisi raha wanayoipata ila kwa upande wao ni tofauti kwa kuwa kila mmoja alikuwa anawaza jambo lake.

Alama ya mawazo ya mume ni makontena yanashushwa na kuna gari inatoka mbio wakati mke anawaza yupo ofisini anasoma ramani kwa umakini sana (picha za mgando zinazotembea).

**Jesca**: Vipi mume wangu, kumbe haujapata usingizi? (Aliuliza akiwa anamgeukia mumewe ili waangaliane).

**Kelvin**: (Anapiga mwayo wa uongo akijizuia na mkono mmoja na mkono mwingine ulimpokea Jesca) Ndiyo nilikuwa napitiwa na lepe la usingizi hapa hivyo umenishtua.

**Jesca**: Afadhali nilale mie…….! (Alitabasamu)

**Kelvin**: Na hayo uliyoyachokoza, utalala vipi?

**Jesca**: Nini?

**Kelvin**: Maongezi

**Jesca**: Mmh! (alimzuia mdomo kwa kutumia kidole cha shahada na kumwambia kwa sauti inayoimbia puani); tulale.

*Walitabasamu.*

**Kelvin**: Sawa lakini rudi ulale vile vile.

**Jesca**: (Aligeuka kimya kimya na kumpa mgongo mumewe kisha kulala akikumbatiwa taratibu).

**Kelvin**: (Alitengeneza shuka na kumfunika mkewe kisha nae aliingia kwenye nguo hiyo. Alijiegesha juu ya mto wake na kulala).

****

Saa kumi na moja Alfajiri simu iliita. Ilikuwa simu ya Kelvin;

Anaonekana Kelvin yupo mlangoni anatokea chooni kavaa taulo, anajinyoosha. Simu iliita tena, alishtuka na kuikimbilia. Kisha kuipokea kwa haraka. Alimwangalia Jesca aliye bado usingizini.

**Kelvin**: Hello, niambie….!

**Simu**: (Anasikiliza huku anajishika shika kifuani akiwa anapiga mwayo.)

**Kelvin**: Umefika tangu saa ngapi? (Aliongea kwa furaha na wasiwasi mwingi) ….Sasa umeshawasiliana na jamaa?

Upande wa simu ulionesha kutoa ufafanuzi uliomfanya Kelvin kukasirika na mara nyingine kutabasamu. Alikuwa amesimama na kuamua kukaa sofani. Mara kwa mara alimwangalia Jesca kwa jicho la wasiwasi.

**Kelvin**: Sawa, poa…… poa…… najiandaa hapa haraka, nikukute nje pale. Tena mwambie dogo niwakute nyote.

Alikata simu na kuonesha vidole kuwa anajipangia ratiba kisha alielekea bafuni badala ya kitandani.

****

Jesca aliamka na kuinuka kukaa kitako, akimwangalia Kelvin aliyekuwa kwenye harakati za kushindilia mavazi haraka haraka.

**Jesca**: Kulikoni?

**Kelvin**: (Aligeuka na kumuangalia mkewe) na wewe umeshaamka? Habari za asubuhi mke wangu?

**Jesca**: Nzuri, kumbe ulinitoroka? Usingizi mwingine huu unaweza kuibwa mume.

**Kelvin**: Mmh! Usingizi wenyewe wa jicho moja moja huo?

**Jesca**: Nini, kisungura?

Walicheka.

**Kelvin**: Kumbe unajua. Nimepigiwa simu na Kanu anasema kontena zile…! Zimefika usiku ndiyo hapa nawahi wasije *kunipiga* tena. (Anavaa viatu vyake akiwa bado amekaa sofani) …. Vipi wewe? Jiandae tutoke sote.

**Jesca**: (Aliiangalia saa) ……Usiku wote huu, wewe nenda tu. Hongera sana, sasa mzigo upi….? Maana umeniambia mizigo mingi. (Aliongea kwa furaha).

**Kelvin**: Kutoka Afrika Kusini.

Kelvin alijibu bila kumuangalia Jesca. Alipomaliza kuvaa, alikusanya simu na funguo toka mezani kisha kumfuata Jesca kitandani na kumbusu.

**Jesca**: Asante. Kazi njema mume wangu. Nitakupigia nikiwa natoka au nikifika kazini ili nijue mambo yamekwendaje (aliongea akiwa amemshika mikono) ……..umesahau simu nyingine…. Ile pale unaichaji (alimuonesha).

**Kelvin**: Asante mama! Namba nyingi zimo humu (anaiokota) ningekwenda kushangaa shangaa tu huko. Nakushukuru (alimfuata na kumbusu tena kisha aliangalia saa ya mkono) ……. Baadae (aliaga na kuondoka).

****

# SURA YA PILI

## Gharama ya siri

Anaonekana JESCA yumo ofisini anafungua mafaili kwa umakini na kuyasoma na kila faili lilikuwa na ramani kama sio juu kwenye jalada basi kwenye karatasi za ndani.

Mara alipigiwa simu baada ya kusikiliza na kukata, alitoka nje na kupanda gari yake na kuondoka.

Akiwa kwenye gari anatoka kuelekea mitaani, simu iliita tena na sasa alikuwa Kelvin.

**Jesca**: Hello.

**Kelvin**: Niambie 'my, ulishafika kazini?

**Jesca**: Ndiyo ingawa nataka nitoke hapa, nimepigiwa simu na wateja wetu wanahitaji nyaraka fulani.

**Kelvin**: Kwanini wasizifuate wenyewe hadi uzipeleke wewe?

**Jesca**: M-m-m (alipatwa na kigugumizi) …..sio niwapelekee tu bali nikaziwasilishe……. Wanakikao….

Mimi nilisahau…. Wamenikumbusha….. vipi wewe…… uko wapi?

Aliongea kwa kubabaika na mawazo mengi kichwani sababu alionesha kusahau aliyoyazungumza.

**Jesca:** (moyoni) Uongo huu….! Unagharimu sana.

**Kelvin**: Nakaribia kufika ofisini kwako nilijua utakuwepo ili nije kukupa mrejesho kwa kukusimulia ana kwa ana. (Aliwasha gari na kuingia barabarani).

**Jesca**: Oh! Karibu, utanikuta na kusubiri halafu nitatoka baadae. Nitawaambia waanze kwanza, nitawakuta kikao kikiwa kinaendelea. (Aliongea kwa pupa).

**Kelvin**: Poa, nakuja.

**Jesca**: Mungu wangu! Sasa hapa…!

Alijisemea moyoni na kugeuza gari haraka na kuingia barabara nyingine na kuibuka nyingine tena kukwepa foleni.

Ghafla, anakutana na foleni ndefu. Aliangaika kuangalia huku na kule labda anaweza kupata upenyo lakini alikosa

na kuona hoteli ipo pembeni mwa barabara. Wazo likamjia la kuacha gari hotelini na kupanda mwendokasi. Alipaki gari na kutoka mbio.

**Mlinzi**: (Alisimama ili kumpokea mgeni na kuishia kushangaa).

**Jesca**: Nakuja sasahivi niangalizie gari yangu.

Alimwambia mlinzi bila ya kusubiri jibu la ndiyo au hapana toka kwa mwenyeji wake. Alipanda mwendokasi na kuondoka.

Kelvin nae yumo njiani anawahi kufika ofisini kwa Jesca.

**Kelvin**: (Alikutana na foleni) ….Mmh! Sasa hapa nafanyaje? Nikisubiri nitamchelewesha Jesca. Sijui nichukue Bodaboda? Na mimi, huu wivu mwingine utaniua.

Mara foleni ilianza kufunguka na magari kuanza kutembea kidogo kidogo. Wazo la Bodaboda lilififia lakini bado moyo ulimdunda na kupiga honi ovyo.

**Kelvin**: Madereva wengine sijui vipi? Kama hawajui kuendesha magari kwa ufasaha, wanakuja vipi ‘high way? Tunacheleweshana tu. (Aliongea peke yake)

****

Jesca aliteremka kwenye mwendokasi na kuchukua Bodaboda hadi ofisini. Alipofika ofisini hata kabla hajaingia ndani, alikutana na watu kwenye ushoroba wa jengo hilo na kabla ya kusalimiana nao mara alionekana Kelvin anaegesha gari nje ya jengo la ofisi hiyo.

Mapokezi;

**Kelvin**: Habari yako dada, ninashida na Jesca.

**Sekretari**: Yumo ndani…… tena…..!

**Kelvin**: Ngoja nimuwahi kabla hajatoka.

**Sekretari**: (Alishangaa) Kutoka? Wakati kaja sasa hivi? Mmh!

Aliongea kwa sauti ya chini kisha aliinua mabega kuonesha hayamhusu.

Anaonekana Kelvin anaingia ofisini kwa Jesca;

**Kelvin**: Pole mpenzi wangu kwa kukucheleweshа. Unajua tena jiji letu hili halina mahali karibu. Kote ni mbali.

**Jesca**: (huku akitabasamu) Karibu. Nilijua upo katika foleni lakini haujachelewa sana hadi kufikia kuomba msamaha. Karibu ukae, (alimpokea mfuko alioubeba kisha aliufunua na kuangalia kilichomo ndani). Ulijuaje kuwa nina kiu sana? (Simu ya Jesca iliita) Karibu hapa…..! (Alimuonesha sehemu ya kuketi Kelvin halafu alipokea simu yake ya mkononi); Hello! Nitafika hapo baada ya dakika ishirini hivi, ninamgeni ofisini.

**Kelvin**: (Alionekana kuwa na hasira)

**Jesca**: Niambie mpenzi wangu……! (Alimfuata na kwenda kuketi karibu yake).

**Kelvin**: Simu zako hizo! (Alihamaki).

**Jesca**: Na wewe, Kwani si ulisema umeweka alama au uongo? (Alijifanya kutojali hasira za mume wake).

**Kelvin**: (Alijilazimisha furaha na kujibu); Haya bwana.

**Jesca**: Hatuaminiani siku hizi?

**Kelvin**: Imani inaponya

Walicheka.

Wanaonekana Jesca na Kelvin wanazungumza kwa furaha na mziki wenye kuvuta hisia za mapenzi na sifa ukisikika kuashiria mafanikio makubwa. Mwishowe anaonekana Kelvin anamuaga Jesca kisha kufungua mlango nakuondoka.

**Jesca**: (Alishusha pumzi) Oh……uuh! (alijishika kichwa) leo ningejulikana…… aibu gani hii….. sasa ngoja nikaendelee na kazi.

Jesca alitoka nje ya ofisi mbio na kumchungulia mumewe kupitia dirishani ili kuweza kuthibitisha kama kweli ameondoka na kuona gari yake inaingia barabarani. Alishusha tena pumzi ndefu.

****

Milango ya saa mbili usiku Kelvin anarudi nyumbani, anaonekana anafunguliwa geti na mlinzi na kupaki gari.

Halafu mlinzi alipofunga geti alikimbilia alipo Bosi wake ili kupokea maelekezo. Walifungua buti ya gari na kutoa mifuko michache.

**Kelvin**: Salama hapa?

**Mlinzi 2**: Salama tu, hamna shida. (Alijibu kwa upole na kujiamini)

**Kelvin**: Mama amerudi? ‘Ok’…..!

Alioneshea kidole gari alilotumia mke wake kuendea kazini baada ya kuiona imeegeshwa sehemu yake;

**Mlinzi 2**: (Huku akitabasamu) yumo ndani.

**Kelvin**: (moyoni) “Nisingemkuta leo angenitambua. Sikutaka kupiga simu makusudi. Nae ananijua nikikasirika.”…. Kaweke stoo mifuko yote hii.

Kelvin alimwelekeza mlinzi akiwa anamuonesha mifuko iliyorundikana ardhini. Alibonyeza simu, kisha aliingia ndani na kuungana na Jesca

**Jesca**: Karibu.

Alimkaribisha akitokea chumbani na kumkuta Kelvin ameshafika sebuleni.

Kelvin: Asante, mbona haukunishtua turudi sote?

**Jesca**: Aah! Nimerudi mapema sana, hata chakula cha mchana nimepata hapa.

Alimpokea kwa kumvua koti kisha kuchukua begi la mkononi lililo bado mkononi mwa Kelvin na kuvipeleka chumbani.

Anaonekana Kelvin kujibwaga kwenye sofa;

**Jesca**: ‘What’s wrong’?

Alishangaa alipogeuka na kumuona mumewe amekaa badala ya kumfuata chumbani.

**Kelvin**: Nakula kwanza, nikioga nalala.

**Jesca**: Sawa.

Anaonekana Jesca anaingia chumbani na kutoka haraka. Wanaelekea mesini na kupata chakula cha usiku kimya kimya.  Kelvin anavunja ukimya na kuuliza;

**Kelvin**: Umesema ulirudi tangu mchana? Kulikoni?

**Jesca**: Ndiyo. Nilipotoka katika kikao tu, kwanza sikusubiri kikao kiishe. Nilipomaliza kuwasilisha tu nikaondoka kurudi ofisini. Sikuwa na kazi nyingine leo, unajua tena biashara siku hizi sio kama zamani.

**Kelvin**: Hata kwenu? Nilishakuambia sasa hivi unatakiwa kurudi nyumbani ufanyekazi katika kampuni yetu. Wewe umeng'ang'ania kwa hao Wahindi wako. 'Deal' siku hizi hamna……! (Alisogeza sahani kando kwa hasira kuashirika anayoyaongea yanatoka moyoni) …..au unataka hadi mpewe 'lidandance?' Hamtopewa. Wanahela sasa yakuwalipa?

**Jesca**: Mume wangu, nimekuelewa (alijibu kwa upole) nipe wiki moja tu kila kitu kitakuwa sawa. Mimi niliona tukiwa tunafanyakazi pamoja nitakufanya usiwe huru katika kusimamia majukumu yako sababu; mfano nikikosea pamoja na wafanyakazi wengine, utanifanyaje? Na endapo ukikaa kimya kwa kuogopa kuniaibisha kazi zitakwenda vipi? Ni hilo tu mpenzi wangu, kula tukalale.

**Kelvin**: (Alisogeza sahani tena)…. Kwani wewe unataka kuja kukosea?

**Jesca**: Ikitokea kwa bahati mbaya na mimi ni binadamu.

**Kelvin**: Kwani nyumbani haukosei?

**Jesca**: Mmh, yamekuwa hayo? Umeshasema nyumbani.

**Kelvin**: Wiki moja unadhani ni nyingi? Njia ya muongo ni fupi, safari hii nisisikie chochote unajifanya kujitetea. Unataka kuaibishana tu, mara mke wa Kelvin katimuliwa kazi unadhani jamii itanielewa?

**Jesca**: Yaishe mpenzi wangu, kula tukalale. Haujafika chumbani ….Leo nilirudi mapema. Kwa sababu……!

**Kelvin**: Aah! (Alitabasamu) hapo umenena mimi nimeshashiba. Nipe 'surprise'. (Aliinuka na kujishika kifua kama anakumbatia kitu).

Wanaonekana wakiinuka na kuelekea chumbani wakishikana mikono na kuchezeana hadi wanaingia chumbani kwao. Kumepambwa vizuri sana.

**Kelvin**: Waooh! (Alimbeba Jesca na kumtupia kitandani).

****

## SURA YA TATU

### Pendo

Waliamka mapema wote kwa pamoja;

**Kelvin**: Vipi 'baby' upo, sawa?

Alikuwa bado kalalia mto na ameweka mikono yote miwili juu ya shuka aliyojifunika.

**Jesca**: Niko poa. Kumbe kumeshakucha hivi? (aliitumbulia macho saa yao ya ukutani)

**Kelvin**: Mmh! (alimtazama na kutabasamu) sasa sikia mama, leo ninasafari kidogo nakwenda Arusha natarajia kurudi baada ya siku mbili…..sa…!

**Jesca**: Mbona ghafla?

**Kelvin**: Hicho ndicho kilinifanya jana nije ofisini kwako nikueleze lakini nilipotezea sababu ilikuwa bado sina uhakika nawe haupendi vitu kama Hivyo. Kifupi nimepata oda nyingi, inabidi kufanya mikataba na baadhi ya watu (wateja). Pia kuna watu ninawadai halafu wanasumbua sana. Unakumbuka yule jamaa wa Noah na yule wa zile

IST, hadi leo hawajamaliza deni …..sasa mbichi ama kavu nitakwenda kupambana nao huko huko.

**Jesca**: Sio ukachokeze ugomvi huko? Nenda kadai lakini fuata taratibu, huko ni kwao.

**Kelvin**: Watanifanya nini? Mimi mwenyewe ni mtoto wa mjini.

**Jesca**: Mmh! Unavyojiamini, haya sawa ……kwa hiyo utaondoka saa ngapi? Kwani umesema leo au kesho?

**Kelvin**: Sasa hivi nikitoka hapa napita ofisini kisha naanza safari mdogo mdogo. Naomba niwekee suruali mbili na mashati au hata fulana tu zinatosha.

**Jesca**: Sawa, ngoja nikuandalie hata nami nataka niwahi kazini. Jana nilitoka mapema sana. Tambua umakini unahitajika safarini na uendako.

Wanaonekana wakiinuka kitandani, Kelvin anaelekea bafuni na Jesca anapanga nguo kadhaa kwenye begi dogo la mume wake pamoja na vifaa vyake muhimu. Kelvin anaonekana anaweka kitita cha fedha katika droo

ya kabati, zinaonesha kuwa nyingi. Wanaonekana wanavaa kujiandaa kutoka;

**Kelvin**: Utawaagiza, hapana…..! Uwapeleke vijana wako wakafanye manunuzi. Pale tulipochukua chakula mara ya mwisho ni pazuri zaidi.

**Jesca**: Wewe si unapenda kule kwa Mzee wako Yule, sijui alikuroga? Yaani hata ukute chenga tupu …..utanunua tu mchele huo hadi jamaa aliniona namzibia riziki nilipotia neno.

**Kelvin**: Yule ni sahibu yangu. Katika maisha lazima uwe na marafiki tofauti tofauti sio kila siku wanyonga tai tu. Ana stori za ajabu yule hadi nahisi zingine za uongo

Kicheko!

**Jesca**: Hizo hizo za uongo lakini zimekuteka mawazo.

**Kelvin**: Siku moja aliniambia alikuwa na kimada wa Kihindi sasa kila akimwambia uhusiano uishe, anaangua kilio! Sasa jiulize waliachana vipi?

Kicheko!

**Jesca**: Labda bado anae……!

**Kelvin**: Aah! Wapi? Mkewe ni mweusi tii! Mimi mweupe. Siku nyingine anakuwepo dukani anawasaidia vijana.

**Jesca**: Ulijuaje kama ndiye mke wake?

**Kelvin**: Alinitambulisha. Hata hivyo nae sio mbaya kivile….! Yuko poa. (alimwangalia Jesca aliyesimama na begi mkononi) Vipi huko tayari? Tuondoke zetu nichukulie funguo zangu hizo hapo juu ya mto (alionesha).

Wanaonekana wanatoka nje, begi amebeba Jesca na ‘hand bag’ ya Jesca ilibebwa na Kelvin. Wanaonekana kubadilishana walipofika nje ya nyumba. Wanaingia kila mmoja garini baada ya kupeana busu na kutakiana heri ya siku na safari.

Kimya kimya;

Magari yanatoka nje na kuingia barabara kuu na siku ilianza namna hiyo.

****

## Raha ya kazi

Jesca yupo ofisini na mfanyakazi mwenzake;

**Jesca**: Hivi yale majalada ulishamaliza kuyaandikia? Siku za kupeleka ripoti zinakaribia. Tusijisahaulishe halafu tusubiri siku za mwisho zifike ndiyo tuanze kuangaika.

**Kesi**: Kila kitu kipo vizuri. Nilikuwa nakusubiri twende Bagamoyo, kuna sehemu moja nimearifiwa kuwa ndiyo kijiwe kikubwa cha hawa watu wetu tunaowafuatilia.

**Jesca**: Aah! Kweli?

**Kesi**: Ukweli tutakwenda kuujulia huko huko tukishafika. Nenda kaonane na Bosi halafu tuondoke zetu. Ingawa inatakiwa tuzuge zuge kwanza mjini hadi jioni hivi sababu mambo hayo hufanywa pindi giza linapoingia.

**Jesca**: Sawa Mkuu, subiri nimuone Bosi halafu tuyapange vizuri sababu itabidi niende nyumbani kwanza.

**Kesi**: Kufanya nini, una mtoto mchanga?

**Jesca**: Nyumbani kuna mengi.

**Kesi**: Haya ndiyo mambo ya wanawake yanayokataliwa. Mkiambiwa mnaanza kudai usawa. Mumeo hayupo nyumbani, wewe unataka ukafanye kitu gani? (Aliongea kwa dhihaka ingawa alimaanisha).

**Jesca**: Nilikutania tu, nilijua utakasirika (alijisemesha baada ya kuona Kesi amehamaki) sasa kwani mume wangu amesafiri na nyumba?

**Kesi**: Si ukamuage! Sijui kuagana? Lakini nadhani tutarudi leo leo ingawa itakuwa usiku sana. Tutatumia gari ya ofisi na tayari nimeshaliandaa.

**Jesca**: Sawa tupo pamoja, hicho ndicho ninachokupendea …..uko chap (aliongea kwa maringo na kufunga mlango kuelekea ofisini kwa Bosi wao).

**Kesi**: (Anajisemea moyoni) Jesca ni mzuri jamani! Kweli wakubwa wanafaidi. Haya…..! (Alishtuka na kutazama huku na kule kuangalia kama sauti ilisikika na kuna mtu amemsikia kisha alikaa vizuri kwenye kiti ili kuendelea na mawazo yake); ananitega kweli ….dah….. nikimwambia tu, tayari nitakuwa nimeharibu kazi. Ngoja nife na tai shingoni. Kazi nyingine hizi ni ngumu sana…….! Ugumu

mwingine ni kama huu ….. yaani haya ndiyo mazingira magumu ya kazi. Kikosi maalum na “sambwanda” hivi ni haki?

Ghafla mlango ulifunguliwa na Jesca anaingia ofisini:

**Kesi**: Mmh tayari eh? (anajilazimisha kuwa ‘serious)

**Jesca**: Yaap! Naweza kukaa?

**Kesi**: Hapana. Tuondoke.

**Jesca**: Sawa.

Walikusanya vitu vyao, vingine walifungia katika madroo ya makabati na meza kisha walitoka nje.

Wanaonekana wapo barabarani wanachanja mbuga kuelekea Bagamoyo na tayari jua lilishatua. Magari barabarani yameshawashwa taa. Kabla hawajafika mahali wanapokusudia kwenda wanayaona magari mawili yamepaki gizani na ndani yake wamo watu.

**Jesca**: Punguza mwendo. Unawaona waleee! (Alionesha)

**Kesi**: Nimewaona. (Alifikiri jambo kwa haraka bila kupunguza mwendo)

**Jesca**: Sasa mbona unazidi kwenda tu tena kwa mwendo kasi? (Aliuliza kwa jazba kidogo).

**Kesi**: Tukipunguza mwendo, watashtuka kama tunachofikiri ndicho wanachokifanya. Wewe tulia, wale hawana ujanja wa kututoka. (Alijibu kwa kujiamini)

**Jesca**: Basi ingia barabara hiyo

**Kesi**: Poa.

Kesi aliingiza gari barabara ya pili na walielekea walikotoka na walipokaribia katika windo lao walipunguza mwendo na kujifanya wamesimama kama gari imeharibika. Kesi alizunguka gari haraka na kufungua bonet kisha alifunika. Muda huo aliutumia Jesca kusoma mazingira kama kweli ni ya kazi au watu wanafanya starehe au mazungumzo ya kawaida. Ghafla alitoka na alichokiona hakuyaamini macho yake na kumfanya moyo wake kushtuka na kuanza kudunda kwa kasi; pale alipomuona mtu mmoja anatoka na mfuko na kuingia

katika gari nyingine kisha gari kuondolewa kwa kasi sana. Kilichomstaajabisha Jesca na kummaliza nguvu ni baada ya kusoma namba za gari iliyobaki si jingine bali ni gari yao anayoitumia mumewe.

Jesca aliona cheche zikitembea usoni na kujikuta anayumba na kudondokea juu ya kiti.

**Jesca**: Ninaota au kweli? (Alijisemea)

**Kesi**: Ile ni kazi. (Aliongea kwa mnong'ono bila kuangalia, alishtuka alipokosa ushirikiano wala jibu.) Ah! Huyu mwanamke ameshatoka? (Alijisemea…. kugeuka! Anamkuta Jesca katumbua macho, kalegea).

**Kesi**: Wewe vipi?

**Jesca**: Gari ni ya mume wangu.

**Kesi**: Mungu wangu! Sasa….? Tufanya haraka akina Sele wapo huku huku doria, wakiliona hili litakuwa bonge soo. Twende haraka.

**Jesca**: Sasa itakuwaje?

**Kesi**: Vaa 'mask' yangu ipo hapo nyuma.

Kesi alitoka na kukimbia kwa kasi akitoa amri ya kusimama na kutofanya chochote. Wakati huo tayari mshukiwa alishawasha gari tayari kwa kuanza safari.

Gizani walionekana watu wawili wakikabidhiana vitu. Wakiwa kwa pembeni kidogo kiasi cha kufanya kutosikika yanayoongelewa ukiwa kwenye magari hayo. Watu hao walionekana kuwa na wasiwasi mkubwa. Sababu walikuwa wanaangaza macho kila upande kila mara kwa aliyekusudia kuwafuatilia anagundua ipo namna.

****

# SURA YA NNE

## Utaweza?

Mwenye gari anatoa gari kwa kasi ili atoroke baada ya kuhisi hali ya usalama juu yake inaanza kutoweka. Anakutana na mdomo wa bastola upo usawa wa kichwa chake. Alijaribu kulazimisha kuondoka hivyo hivyo ikiwezekana amkanyage mwenye bastola sambamba na kukataa kushusha kioo cha gari lakini alitaharuki alipoona gari haitembei ingawa alikanyaga mafua hadi mwisho. Mashine ililalamika bila ushirikiano wa safari. Kumbe tairi zote za nyuma na mbele zilikuwa hazina upepo. Gari ilizimwa na dereva alifungua mlango wa gari na kupiga magoti kuomba msamaha.

**Dereva** (Kelvin): Naomba mnisamehe….. nilighafilika!

**Kesi**: Kughafilika nini?

**Dereva**: Nilijua majambazi

**Kesi**: Kumbe sisi ni nani?

**Dereva**: Siju….. sijui…. Mkuu naomba unisamehe.

Kabla ya kuendelea kujitetea aliletwa binti (mrembo) aliyevaa nguo ya kubana na kumpendeza sawia kabisa. Kesi alikuwa amechanganikiwa sababu hakujua mwenzake ana mawazo gani juu ya washukiwa wake. Je, ni mambo ya kazi au mapenzi? Sababu ilikuwa ngumu kumsoma kwa kuwa hadi muda huo, Jesca alikuwa hajatia neno.

**Kesi**: Ulikuwa unampa nini yule kijana aliyeondoka? (Aliuliza kwa sauti ya ukali na ngurumo kama radi)

**Dereva**: Nani? yu….yupi?

Alishtukizwa na kibao cha nguvu kilichompeleka chini hadi kumfanya mrembo wake kutoa sauti ya uchungu.

**Binti**: Yesu wangu! Naomba mumsamehe Mpenzi wangu.

Aliomba msamaha akiwa amepiga magoti ardhini akifikicha viganja vya mikono. Ghafla nae alipigwa kibao cha kerebu na kumpeleka chini bila kuinuka wala kufumbua macho.

**Kesi**: Tuambie umempa nini yule?

**Dereva**: Fedha….. fedha… ni kijana wangu ninamtumia kufanya biashara.

**Kesi**: Kwanini mlikuwa mnapeana fedha gizani?

**Dereva**: Sikutaka watu waone sababu fedha zile ni nyingi wangeweza kumpora.

**Kesi**: Unajifanya mjuaji eh? ……Unafanya biashara gani?

**Dereva**: Nanunua mazao vijijini.

**Kesi**: Mazao gani?

**Dereva**: Mpunga, maharage, viazi ……!

Alipigwa teke la tumbo na Jesca. Alianguka chini kama furushi na kutoa mguno wa maumivu.

**Kesi**: Wewe sio unafanya biashara za kikahaba? Huyu ni nani?

Alimuonesha binti ambaye alikuwa bado amelala baada ya kipigo.

**Dereva**: Huyo ni mke wangu.

**Kesi**: Mke wako? Ndiyo anavaa hivi? Mbona wewe umevaa vizuri? Ninyi ndiyo mnaofanyakazi za kuwadhalilisha wanawake na wasichana. Kwanza huyu binti anaonekana ni mtoto inawezekana ikawa ni mwanafunzi.

**Dereva**: Naomba mchukue fedha nyingine zimo humo chini ya kiti muondoke nazo, mtuachie roho zetu mtoto wetu hatabaki mkiwa mkituua. Alijiinua kwa shida na kwenda kumuangalia mpenzi wake.

Anaonekana Jesca anaingia katika gari na kuchukua fedha kisha kupeana ishara ya kuondoka. Dereva (Kelvin) anamburuza binti na kumweka kwenye gari na kuanza kupiga simu ya kuomba msaada.

Kwa bahati mbaya Jesca akiwa anafunga mlango kwa hasira alijikwangua. Walipotoka eneo la tukio, Kesi alimsaidia kumfunga plasta

****

Kwenye gari, Jesca aliangua kilio cha kutisha kana kwamba kapata taarifa za msiba. Kesi alimbembeleza;

**Kesi**: Mimi naona leo tuishie hapa. Tutarudi nyumbani na tutajipanga tena.

**Jesca**: Sawa.

Kesi aliendesha gari na kumtuliza Jesca kwa yote;

**Kesi**: Mama, achana na habari za kulia twende nyumbani halafu tutulie tutafakari yale tuliyoyaona na tupange cha Kufanya. Nakuahidi kushirikiana na wewe. Tupo pamoja! Futa machozi mama. Unajua wewe una akili sana. Kitendo cha kuchukua fedha ndiyo mwisho wake, lazima atarudi nyumbani. Naomba niahidi hatagundua chochote…..! (Alimshika kiganja cha mkono kwa upole huku akimwangalia, akimkazia macho.)

**Jesca**: Na….na nakuahidi. (Alifuta machozi kwa kiwiko cha mkono).

**Kesi**: Sasa kama ni hivyo futa machozi.

Alichukua leso mfukoni na kumpa. Alipoipokea na kuisogeza usoni, Kesi alisema kwa hamaki;

**Kesi**: Aah! Nilisahau kumbe ni kile chenye pilipili……!

Jesca alikitupa kitambaa juu kwenye dash board haraka.

**Kesi**: (Aliangua kicheko na kusema); Askari mzima unaogopa pilipili?

**Jesca**: Ah! Umenishtua.

**Kesi**: Pole ‘dear’ nimekutania, haya chukua ni kisafi nilifua jana na kunyoosha leo asubuhi. Umesikia?

Anaonekana Jesca kufuta machozi na kuendelea na safari. Wanafika mgahawani kuchukua chakula‘take away’ kateremka Kesi na baada ya dakika chache anaonekana kurejea garini.

**Kesi**: Naomba ule nikiwa nakuona ili ukifika nyumbani ni kulala tu. Kesho tutakuwa na kazi nyingi.

**Jesca**: Mmh! Mimi sina njaa. Hamu ya chakula imepotea.

**Kesi**: Fungua tule sote.

**Jesca**: Utakulaje ukiwa unaendesha?

**Kesi**: Mama, fungua chakula tule.

Walianza kula huku safari inaendelea Kesi alikuwa anampenda Jesca kiasi cha kumwekea wivu.

Anawaza;

**Kesi**: “Yaani jamaa bwege sana anamuacha mwanamke wa maana huyu anakwenda kuparamia vitoto. Kitoto chenyewe kimekomaa! Make-up tu zile. Sasa aibu iliyompata ni yanini pale? Ndiyo maana J amemwachia, hivi Queen wa ukweli….. huyu leo si angezimia ……..natamani ajue kama nampenda…. Si…!”

**Jesca**: Mbona umeacha kula?

**Kesi**: Nakula mama.Tuendelee.

Anaonekana Kesi anamshusha Jesca nyumbani kwake;

**Jesca**: Kesi, asante sana kwa kunifariji. Asubuhi nitachukua taxi, usiangaike kunifuata.

**Kesi**: Usijali.

**Jesca**: Usiku mwema.

**Kesi**: Nawe pia mama. ‘Take care’.

## SURA YA TANO

### Subra

Mziki, simu inaita chumbani kwa Jesca. Alipoangalia anayepiga, ni jina la mume wake;

**Jesca**: Hello

**Kelvin**: Hello mke wangu!

**Jesca**: Kulikoni unaongea kwa fadhaa, kwema?

**Kelvin**: Kwema lakini ungelisikia tu nimekufa leo na sasa ungelikuwa mjane.

**Jesca**: Eeh! Vipi tena? Nilishakuonya mambo ya ugomvi sio mazuri iweje wewe ukaanza kuparamia watu hadi wanataka kukutoa roho?

**Kelvin**: Sio hivyo mke wangu, naomba nisikilize kwanza. Jana usiku na washikaji zangu tukiwa tunatoka zetu kupata chajio, tulishtuka watu ‘wametu-tight’. Tukanyang’anywa kila tulivyonavyo. Mimi na mwenzangu mmoja wametuchukulia fedha. walituburuza lakini walivyopata wanachotaka wakatokomea zao. Hivyo

nilipelekwa zahanati na sasa sijambo. Ningekuwa karibu ningelisema unifuate sababu kuendesha gari hadi huko siwezi.

**Jesca**: Kwa hiyo utaugulia huko huko hadi upone?

**Kelvin**: Hapana. Nimeshapata dereva wa kukodi, atanileta

**Jesca**: Nashauri urudi nyumbani tena leo hii.

**Kelvin**: Sijui leo nitaweza kukaa katika gari na umbali wote huu?

**Jesca**: Leo kabla halijachwa…… uwe nyumbani. Mimi kupeana 'pressure' sitaki ……nimesema leo. Kwanza na mimi naumwa niliona nikikuambia nitakuchanganya.

**Kelvin**: Lakini wewe haunihurumii hata kidogo! Nakuja mama, nitakuja uniuguze.

**Jesca**: Karibu.

Baada ya kukata simu Jesca alilia sana na baadae alinyamaza na kukumbuka maneno ya Kesi kuwa amemuahidi kushirikiana nae bega kwa bega.

****

Kazini; anaonekana Jesca na Kesi wanaandika taarifa za kazi zao mbalimbali;

**Kesi**: Vipi mama, mambo yanakwenda?

Aliuliza kwa kuvizia ili aweze kujua ‘mood’ ya Jesca ipo vipi?

**Jesca**: Poa…… lakini haya mambo ni magumu……. Yaaani….. sijui? Mmh…! (aliguna na kushika tama).

**Kesi**: Yaani wewe unayazungumzia yale yale ya jana? Mimi si nilikuambia niachie mimi ……..wewe kuwa na amani. Kila kitu nimeshapanga subiri matokeo. Jana mimi sikwenda kulala kwa ajili yako nilirudi kule na hadi sasa ninaijua hoteli waliyofikia na chumba walicholala. Halafu we…..!

**Jesca**: Aah! (Aliinuka kwenye kiti na kwenda kumkumbatia Kesi kwa furaha na kusema) ….Ninakushukuru sana……. Nimeamini kweli una nia ya kunirejeshea furaha yangu.

**Kesi**: Nakupenda sana sitaki nikuone unasononeka. Fanya kazi zako halafu ukishamaliza naomba nishtue. Ninakwenda Mnazimmoja ninaahadi na Afisa mmoja.

**Jesca**: (Uso uliojaa tabasamu na matumaini) Asante sana Kesi. Ninakwenda kuripoti kwa Bosi ndiyo nije endelea na kazi. Sijakwenda kuripoti hadi sasa hivi.

**Kesi**: Eh! Nilijua ulivyojituliza hapo mwenyewe tayari umeshamuona jamaa. (Aliendelea) Sasa kuhusu tukio la jana la mumeo sijaliandikia, sababu ningeandika ni lazima tumfikishe kituoni kwa mahojiano. Ili isituaribie mambo ni bora tuache kwanza tutajua tutalizuia vipi. Lakini mumeo jana alikabidhi madawa ya kulevya na yeye alipewa fedha zake za mzigo uliouzwa. Nimeshajua hadi kijiwe cha yule kijana lakini sijafanikiwa kujua jina kamili.

**Jesca**: (Alionesha tena hali ya kuchoka hadi kushindwa kufungua midomo ili kutoa neno na kubaki kutoa macho kwa mshangao).

**Kesi**: Kama nilivyokuambia niachie mimi tutamhukumu wenyewe kabla ya mahakama. Nijulishe ukimaliza kazi

kama nilivyokuambia. Kula ni muhimu kwa sasa ili usipoteze nguvu.

Aliinuka na kutoka nje akimkonyeza kwa utani kuashiria abaki salama.

**Jesca**: (Aliwaza) …..Huyu mwanaume atanitoa roho. Yaani biashara yake anaona haitoshi na kuanza kujiingiza kwenye kufuru. Amenivuruga sana kwa kitendo aliuchokifanya. Kwanini anafanya vitu vya ajabu kiasi hiki? Ewe Mwenyezi Mungu, naomba umsamehe bure! (Alishika uso na kujizuia kwa kiganja).

****

Majira ya saa sita mchana anaonekana Jesca katika mgahawa anatoka na mfuko mkononi. Anakutana na shemeji yake anayefanyakazi katika kampuni ya Kelvin jina lake ni Bwana Kanu. Ndiye Meneja wa kampuni ya Kelvin.

**Kanu**: Shemeji

**Jesca**: Ah! Mambo vipi? Karibu

**Kanu**: Asante, habari za kwenu uko? Poleni na matatizo

**Jesca**: (Moyoni) “Matatizo?” (fahamu ilimjia) Oh! Asante ndiyo maisha. Wapo wanaotafuta fedha na wengine wanaotafutwa kwa ajili ya fedha. Muhimu na cha kushukuru Mungu ni uzima, fedha zipo tu.

**Kanu**: Aliniambia walishaanza safari ya kurudi sijui watakuwa wapi muda huu? (Alijipapasa mifukoni kutafuta simu yake lakini hakuiona) Ah! uzee huu, kumbe nimeiacha simu kwenye gari. (Alionesha mwelekeo wa alipoegesha gari)

**Jesca**: (Alifuatilia mwelekeo huo kama mazungumzo yao yalivyohitaji na ghafla moyo wake ulimpasuka paa! Alikuwa anaifahamu vizuri gari ya Kanu. Lakini alichokiona ndani ya gari kilimpa fadhaa na moyo ukasinyaa kwa sekunde kadhaa na kujisemea; “Nafananisha au kweli?”

Ndani ya gari kulikuwa na mrembo anayelandana kabisa na yule wa Kelvin aliyempa kichapo jana usiku.

**Kanu**: Vipi shemeji, kuna tatizo?

**Jesca**: Mmmh eh….! Unasema?

**Kanu**: Naomba nikuache tutaongea baadae. Jioni naweza kuja nyumbani kwenu kuwasabahi.

**Jesca**: Karibu Shemeji.

Moyo wake ulikuwa unatamani kuona vizuri lakini kioo cha giza sehemu ya nyuma ilitosha kumfanya Jesca kushindwa kuhakiki jambo lake.

****

Jioni anaonekana Jesca anarejea nyumbani na kumkuta Kelvin ameshafika. Kufungwa bandeji mkononi na mguuni. Anaonekana Kelvin anamkaribisha Jesca kwa furaha ingawa aliipokea kwa hasira na mwenye jazba kiasi cha kupatwa na kigugumizi.

**Kelvin**: Karibu mke wangu

**Jesca**: Pole mume wangu na matatizo, karibu nyumbani. (Hakuonesha kuhuzunika wala kufurahi).

**Kelvin**: Asante sana, pole na wewe. Vipi hapo umekumbana na nini?

Anaonekana Kelvin anakishangaa Kidole cha Jesca kilichofungwa plasta.

**Jesca**: Mapishi hayo. Vipi umeshakula?

**Kelvin**: Niko sawa. Nilipita pale unapopapenda nikapata msosi na kijana kabla ya kuja nyumbani. Nilijua utakuwa kazini.

**Jesca**: sawa. Twende zetu chumbani hata mimi nimekula vikaoni huko.

**Kelvin**: “Asante Mungu, hajagundua kitu chochote. Sijui ingekuwaje?” (Aliwaza)

**Jesca**: Vipi mbona unaongea peke yako?

**Kelvin**: Eeh! (alishtuka) mmh…..! Ninaimba tu nyimbo za kwetu.

**Jesca**: AKhaa! (Alilazimisha tabasamu).

Wanaonekana kufika chumbani. Baada ya muziki, wanaonekana wamelala; Kelvin kapitiwa na usingizi na Jesca amekaa kitandani kashika mto anataka kumziba pumzi mumewe lakini moyo unasita (picha za mnato,

Kelvin akiwa amekufa, maombezi kanisani, makaburini, maombolezo, na mjane analiwazwa). Mwishowe nae anaonekana anaweka mto kitandani nakuamua kulala.

****

Wanatembelea sehemu kupata upepo kidogo kana kwamba hamna yaliyotokea. Walipofika supermarket, mara simu ya Jesca inaita……. Alipokea na kusikiliza.

**Jesca**: Poa. Subiri nipo karibu na ulipo. (Alimgeukia mumewe) Kelvin, kuna mtu natakiwa nimkabidhi nyaraka zimo garini (alilinyooshea kidole). Yupo hapo nje, karibu na banda la maziwa.

**Kelvin**: Tuondoke tu kabisa, kwani kuna cha kuongeza?

**Jesca**: Hapana.

Kelvin alimkumbuka Kesi kuwa ndiye jambazi aliyemvamia usiku Bagamoyo. Alishangaa kuona anajuana na mkewe. Kesi alijifanya hajamuona wala kuhisi wanafahamiana pindi walipokutanisha mboni. Jesca aliteremka garini na kumpa bahasha kisha kurudi kwenye gari yao kuungana na Kelvin aliyesalia humo.

Baada ya Jesca kurudi kwenye gari;

**Kelvin**: Yule ni nani?

**Jesca**: Ni mteja wetu. Vipi mnafahamiana? (Alijibu akiwa anafunga vizuri mkanda wa kiti cha gari).

**Kelvin**: Hapana. Nimekuuliza tu (aliona yasije kuwa makubwa na kuamua kupotezea).

**Jesca**: Tunaelekea wapi sasa, nyumbani au?

**Kelvin**: Yap.  Au tukamtembelee mtoto shuleni kwao?

**Jesca**: Labda kesho jumapili. Leo watatuzuia kumuona

**Kelvin**: Sawa.

****

Nyumbani;

Anaonekana Kelvin anapekua vitu kujiridhisha kama kuna dalili ya kuhusiana mke wake na kijana aliyempa bahasha. Kwa bahati nzuri hakuona chochote chenye kutiliwa shaka. Anaamini itakuwa kweli ni mteja wa kazini kwa mke.

**Kelvin**: Daah! Kweli duniani wawili wawili. Jana palibakia padogo, yaani hivi (alifinya vidole viwili vya mkono) ningefichua siri kwa taharuki.

Baada ya wiki mbili Kelvin aliaga tena kuwa amepata safari ya kwenda Tanga kisha Moshi na atarejea baada ya siku tano.

Anaonekana anapakia begi na vifaa vingine kwenye gari na mlinzi wake.

**Kelvin**: Mke wangu, nakupenda sana.

**Jesca**: Asante nashukuru. Nami nakupenda (maneno haya yalimuumiza sana lakini alijikaza) …kuwa makini sana huko uendako. Yaliyotokea mwanzo jitahidi yasijirudie.

**Kelvin**: Asante mpenzi. Nitazingatia hayo. Nenda umfikishie salamu zangu Junior (Kelvin Mtoto) utakapokwenda kumtembelea sababu Jumapili ile tuliahidi lakini tulikosa kwenda lakini Jumapili hii jitahidi uende. Kamwambie baba yake anampenda sana. Nimeshindwa

kumtembelea kwa sababu nimepata udhuru, ‘Next time’……nitamchukulia mazaga zaga kibao.

**Jesca**: Salamu si mzigo, atazipata. ‘Take care’

Kelvin aliingia kwenye gari na kutokomea.

# SURA YA SITA

## Ni huyu?

Siku ya tatu baada ya safari ya Kelvin

Hotelini;

Anaonekana mtu anagonga mlango wa moja ya vyumba vya hoteli hiyo. Baada ya kufunguliwa, anaonekana KELVIN na mpenzi wake wa chini ya ulinzi wa bastola ya rafiki yake KANU na msindikizaji wake alikuwa KESI. Wanaonekana wanatoka chumbani humo kimya kimya kama watu wenye makubaliano hadi kusikojulikana na ndipo mazungumzo yalipoanza.

Mazungumzo hayo yanaonekana ni amri toka kwa watekaji iliyomtaka Kelvin kujidhuru kwa kujikata kwa kiwembe mwilini mzima hadi alowane damu. Wapendanao hao walilia kwa hofu na maumivu.

Kanu aliongea;

**Kanu**: Yaani Bosi umeamua kumchukua mchumba wangu kwanini? Kama uliona mke wako hakutoshelezi na

unahitaji ziada kwanini uninyang'anye tonge mdomoni? Ukaacha kutongoza wanawake wengine na wala hujawaona hadi umchukue huyu? Endapo nilikukosea katika kutekeleza majukumu yangu ya kazi uliyonikabidhi ni heri ungenifuta kazi kuliko kunilamba kisogo na kunidhalilisha kiasi hiki….!

Alianza kulia na kutaka kuwafyatulia risasi lakini Kesi aliiwahi na kumnyang'anya bastola.

Kanu aliendelea kuomboleza kisha kumrukia Nasra (binti) na kumshika na kumtingisha kama dawa ya maji.

**Kanu**: Nasra unakosa nini kwangu? Unanidanganya unakwenda kumuona mama yako kumbe unatoka na Bosi wangu? Haya sasa huyu ndiyo mama yako? Ninalipa ada na gharama zote za chuoni tangu mwaka wa kwanza hadi sasa upo mwaka watatu. Unajiona tayari umemaliza na kuanza kunifanyizia kwa kuwa mimi ni bwege? Si ndiyo maana yake? Halafu wewe bwege unafanya utani eh? (alimgeukia Kelvin) fanya kama nilivyokuambia usitake nikukate mimi nitakuua!

**Kelvin**: Sa…….sa….wa……Naomba…..u-ni-sa-me-he, sirudii tena.

**Kanu;** Kaburi hakuna mapenzi….!

**Kesi**: Muongo mkubwa! Juzi juzi niliwachapa vibao na leo mmerudia tena. Unataka utolewe masikio yako ya ku'ume ndiyo utakoma? Inaonekana yanakusumbua.

**Kanu**: Unasemaje….? hawa? (Aliwaoneshea kidole)

**Kesi**: Ndiyo hawa!

Hasira!

Anaonekana Kelvin analalamika sana kwa maumivu na kisha NASRA kunyongwa mguu wa kushoto hadi ulionesha kama umevunjika na hapo hapo alilegea na kupoteza fahamu. Baada ya kukamilisha tukio hilo anaonekana Kanu anamlalia Nasra juu ya kifua na kuanza kulia kilio cha kwikwi.

Kesi alimwinua Kanu na kuondoka nae eneo lile hadi mahali walipopaki gari yao kisha kurudi mjini na kuwaacha wawili hao kichakani wakipambania uhai wao.

****

Wanaonekana wagonjwa wapo hospitali wana hali mbaya. Jesca yupo pembeni ya kitanda, analia.

Baada ya siku tatu wagonjwa walipata nafuu ambapo Kelvin aliruhusiwa kutoka hospitali na kurudi nyumbani. Nasra alifungwa kopa kwenye mguu uliovunjika na kuruhusiwa pia. Alishindwa kwenda chuoni kutokana na maumivu.

Anaonekana yupo katika chumba kimoja cha Uswahilini akiwa na Mama yake anampa maji ya kunywa.

**Mama**: Sasa mitihani itakuwaje?

**Nasra**: (Analia …….. anashika simu na kuirudisha chini.)

**Mama**: Ubaya wake kwenye hili, mimi sijui pakuanzia wala kuishia. Kijana uliyemfanyia vitendo vibaya ndiye aliyekuwa anatusaidia na kututunza. Sasa leo kipo wapi? Nilikuonya lakini haukunisikiliza ona sasa yamekutokea puani. (Alipiga makofi yakulemewa) …….Sasa jaribu kuwapigia rafiki zako labda watakusaidia.

Nasra aliendelea kuchezea chezea simu yake ya mkononi. Amepigwa bumbuazi.

****

Nyumbani kwa Kelvin - chumbani;

**Kelvin**: Mkosi gani huu? Inaonekana kuna mtu ananiwinda (Alijikaza kujieleza alipoona mkewe haoneshi kama anajua chochote tangu alipompokea na kumuuguza hospitali hadi muda huo wapo nyumbani, kitanda kimoja! Alijisemea;) “Itakuwa Kanu hajaongea lolote. Nitamtafuta ili tuyamalize.”

**Jesca**: Mkosi gani?

**Kelvin**: Maisha gani haya yenye kuvamiwa na majambazi kila siku?

Aliongea akiwa amelala kwenye kitanda chao kikubwa chenye nakshi za kupendeza.

**Jesca**: Unalikumbuka tukio lenyewe na hao watu unawajua au ukiwaona utawatambua? Kwa maana ninachokijua mimi ulisafiri kwenda Tanga halafu Moshi.

Sasa nilivyoelezwa……. Mimi sijaelewa….. mara wapi…. mara kule ….mara huku….!

**Kelvin**: Nilivamiwa na majambazi nikiwa Bagamoyo. Nilipigiwa simu na Kanu usiku kuwa kuna mzigo wetu utashushwa Bandari ya Bagamoyo hivyo nilitoka kule usiku na kufika pale salama. Muda mchache baada ya kufika; niliwaona watu …….kwanza walinigongea mlango nilidhani ni wahudumu wa hoteli lakini ile kufungua tu! Waliingia na kuanza kudai hela mara hati, basi tafrani.

Jesca alianza kububujikwa na machozi na kisha kilio kiliongezeka lakini hakuongea kitu chochote.

**Kelvin**: Sasa unalia nini mke wangu wakati mimi nipo hai? Fedha zinatafutwa na tutapata nyingine.

Jesca aliendelea kulia ingawa KELVIN alimbembeleza sana bila mafanikio mwishowe alikasirika na kutamani ampige vibao ili alie kwa halali.

**Jesca**: (Aliamua kutumbua jipu) Kwanini unanidanganya una safari za kikazi kumbe unakuwa mjini unakula raha na

vimada? Mimi ninakukera mume wangu hadi unifanyie hivyo?

**Kelvin**: (Alishtuka) Eeeh…..!

**Jesca**: Funua huo mto ulioegemea

**Kelvin**: (Aliinua mto haraka na hakuamini alichokiona)

Ilikuwa picha ya ninja na bahasha ya hela aliyokabidhi kwa majambazi feki.

Akiwa bado hajaelewa kinachoendelea aliulizwa;

**Jesca**: UNAMJUA HUYU? Mimi ndiye niliyemwambia KANU aje kukufumania kwa kuwa unatembea na mchumba wake. Halafu mimi sifanyi kazi kwa Mhindi wala nini ….bali ni Askari wa Kikosi Maalum. Biashara yako ya madawa ya kulevya tayari ipo mezani kwangu.

Kauli za mkewe zilimfanya Kelvin kupatwa na mshtuko na mwishowe alizimia.

Anaonekaka hospitali na 'drip', pembeni yake amekaa Askari Polisi mmoja mwenye sare badala ya mke wake kama ilivyo desturi yao. Kelvin anaweweseka kwa

kuongea maneno ya majuto ya kuwasaliti wapendwa wake na kujihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya. Kwa sababu hakukuwa na haja ya yeye kujiingiza kwenye biashara haramu wakati biashara yake ya halali, ingetosha kumfanya aishi vizuri mjini.

MWISHO